JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MUHTASARI WA RASIMU YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

DESEMBA 2024

# UTANGULIZI

Katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, Tanzania imetekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Dira 2025), ambayo ililenga kuinua uchumi kufikia nchi ya hadhi ya kipato cha kati. Dira hii ilijikita katika kuleta mageuzi kupitia kilimo cha kisasa, viwanda, ujenzi wa miundombinu, na maendeleo ya teknolojia. Hadi mwaka 2020, Tanzania ilifikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya chini, ikiwa na wastani wa kipato cha kila mtu cha Dola za Marekani 1,080, ikiwa ni ongezeko la asilimia 170 tangu mwaka 2000. Viwango vya hali ya maisha viliimarika kwa kiasi kikubwa, huku kiwango cha umaskini uliokithiri kikipungua kutoka asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2022. Sekta za afya na elimu nazo zimeimarika zaidi: udumavu wa watoto chini ya miaka mitano ulipungua kutoka asilimia 48 mwaka 2005 hadi 30 mwaka 2022; vifo vya akina mama wakati wa uzazi vilipungua kutoka 675 mwaka 2005 hadi 104 mwaka 2022 kwa kila vizazi hai 100,000; vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 112 mwaka 2005 hadi 43 mwaka 2022 kwa kila vizazi hai 1,000; na uandikishaji wa shule za msingi ulifikia asilimia 100 mwaka 2020, huku kukiwa na ongezeko kubwa la viwango na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari.

Pamoja na mafanikio hayo, jitihada zaidi zinahitajika kutokomeza umaskini na kujenga uchumi imara na jumuishi. Kuelekea mwaka 2050, Tanzania inadhamiria kufanya mageuzi makubwa ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo yatalingana au kuzidi ya nchi za kipato cha kati ngazi ya juu. Hata hivyo, kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) jitihada zaidi zinahitajika ili kukabiliana na mabadiliko makubwa yatakayojitokeza, ikiwemo ongezeko la idadi ya watu ambayo inatarajiwa kuongezeka mara dufu hadi kufikia milioni 140, zaidi ya nusu wakiwa wanaishi mijini. Mabadiliko haya ya idadi ya watu yataathiri kwa kiasi kikubwa usalama wa chakula, makazi, ajira, elimu, na huduma za afya. Uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu kama vile kilimo, madini, utalii, viwanda, na teknolojia utakuwa muhimu ili kukuza uchumi kwa zaidi ya mara nne ili kukidhi mahitaji ya kijamii ya wakati huo.

Wakati huo huo, Tanzania italazimika kukabiliana na mabadiliko kadhaa yanayojitokeza duniani, ikiwemo ongezeko la tofauti za kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi, ukuaji wa miji, teknolojia zinazoibuka, na mivutano ya kijiopolitiki. Hata hivyo, fursa za kimaendeleo zinaendelea kujitokeza kama vile maendeleo ya kiteknolojia, mabadiliko ya ulimwengu kuelekea nishati safi, na usawa wa kijinsia unaoongezeka. Kwa kutumia idadi kubwa ya vijana wake, rasilimali asilia, na nafasi yake ya kijiografia, Tanzania inaweza kuendeleza ustawi wake huku ikichangia malengo ya maendeleo endelevu duniani.

Dira 2050 inaweka maono makubwa kwa mustakabali wa taifa na mikakati ili kufikia mandeleo. Dira 2050 inajengwa juu ya mafanikio na uzoefu wa utekelezaji wa Dira 2025 na kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali duniani. Dira 2050 inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye nguvu kiuchumi barani Afrika na duniani kwa ujumla. Dira italiongoza taifa kuwa na mustakabali endelevu, unaozingatia usawa, hususani wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, na ustawi wa watu wake wote.

## *Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea*

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) inalenga kuwa na taifa ***jumuishi, lenye ustawi, haki, na linalojitegemea*** kuelekea mwaka 2050. Dira 2050 inaweka mkazo katika maendeleo ya watu, kutokomeza umasikini wa aina zote, na kujenga taifa lenye uchumi imara, jumuishi, na shindani utakaoboresha maisha ya watu.

### Misingi ya Dira

1. **Umoja:** Kila Mtanzania ana jukumu la kudumisha Muungano, umoja na mshikamano wa kitaifa.
2. **Utu:** Kila mtu anastahili kuheshimiwa, kuthaminiwa na kulindwa utu wake;
3. **Uhuru na Haki**: Kila mtu anahitaji kufurahia haki zote na uhuru na kulindwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
4. **Demokrasia:** Kila mtu, jamii na taifa kwa ujumla lina jukumu la kuheshimu, kulinda na kudumisha misingi ya demokrasia, utawala bora, utawala wa sheria na kuzingatia Katiba.
5. **Ulinzi wa Maliasili na Rasilimali:** Ulinzi na matumizi endelevu ya maliasili na rasilimali za Tanzania ni msingi wa maendeleo ya watu wake. Hivyo, maliasili na raslimali za taifa zitalindwa, kusimamiwa, na kutumiwa vema kwa maendeleo endelevu na ustawi wa taifa, na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.
6. **Ulinzi wa Utamaduni na Maadili ya Taifa**: Urithi wa utamaduni wa Tanzania na maadili ya taifa vitahifadhiwa, kukuzwa na kulindwa ili kujenga utambulisho wa kitaifa na umoja, na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

### Malengo ya Dira 2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo inadhamiria kufikia malengo yafuatayo ifikapo mwaka 2050:

1. Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu, yenye uchumi mseto, stahimilivu, imara na jumuishi.
2. Kutokomeza aina zote za umaskini, hususan kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, sambamba na kuimarisha maendeleo sawia kimkoa.
3. Kuwa na ubora wa hali ya juu wa maisha na ustawi kwa wote.
4. Kujenga kikamilifu uwezo wa rasilimali watu hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuchochea maendeleo ya taifa na kushiriki kama raia wa kimataifa wenye ubunifu, fikra tunduizi, na kujiamini.
5. Kuwa na mfumo imara wa utawala uliojumuishi, wenye uwazi na unaohakikisha amani ya kudumu, uhuru na usalama wa watu.
6. Kuwa na mfumo imara na endelevu wa usimamizi thabiti na endelevu wa ikolojia na rasilimali ili kujenga ustahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi.

## SHABAHA ZA DIRA

Kuelekea 2050, Tanzania imeweka shabaha zifuatazo:


1. Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati ngazi ya juu, ikichagizwa na sekta ya uzalishaji viwandani. Lengo ni kufikia pato la mtu, kati ya Dola za Marekani 4,700 na 8,000, na pato la taifa kufikia zaidi ya bilioni 700 za Dola za Marekani ifikapo mwaka 2050.
2. Kuondoa umaskini uliokithiri na kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji kuwa chini ya asilimia 5.
3. Tanzania kuwa nchi kinara katika uzalishaji wa chakula barani Afrika, na kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa kumi wa chakula duniani.
4. Kuwa na mazingira bora ya kufanya biashara, na kushika nafasi ya tatu bora barani Afrika katika kuvutia wawekezaji.
5. Kuwa na sekta binafsi imara na yenye ujasiri na uwezo wa kushindani kikanda na kimataifa.
6. Kiswahili kuwa lugha inayoheshimika na kutumika kama moja ya lugha mbili rasmi katika ukanda wa Afrika na moja ya lugha rasmi zinazotumika katika Jumuiya ya Umoja wa Mataifa.
7. Kuwa na mfumo bora wa elimu katika ngazi zote unaojenga maarifa na stadi za wahitimu na wenye kushabihiana kwa karibu na sekta za uzalishaji.
8. Kuwa na jamii yenye afya njema ambapo kila mtanzania anapata huduma bora za afya, maji na hifadhi ya jamii.
9. Kuwa taifa linalojitegemea katika mahitaji ya umeme ambapo wastani wa matumizi ya umeme kwa mtu yatakuwa angalau kWh 600.
10. Kuwa na jamii inayothamini uhifadhi wa mazingira na iliyo tayari kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.
11. Tanzania kuwa kitovu cha huduma za usafirishaji mizigo ya kibiashara katika ukanda wa Afrika.
12. Kuwa na jamii yenye maarifa ya kidijiti na yenye uwezo wa kutumia zana na kuzalisha teknolojia za kidigiti katika huduma na uzalishaji.
13. Tanzania kuwa taifa la kidemokrasia, likiongozwa na katiba imara inayoakisi mwafaka wa kitaifa, taasisi madhubuti za umma, na mfumo thabiti wa vyama vingi vya siasa.
14. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora duniani na kushika nafasi ya kwanza barani Afrika katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2050;
15. Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kwa wanaume na wanawake kufikia miaka 75;
16. Tanzania kuwa nchi kinara barani Afrika kwa vivutio vya utalii na miongoni mwa nchi tatu bora barani Afrika zinazotembelewa na watalii kwa wingi;
17. Kila Mtanzania kuwa na elimu angalau ya kidato cha nne, na angalau asilimia 15 ya Watanzania kuwa na elimu ya juu, wakiwa na ujuzi stahiki unaolingana na mahitaji ya soko la ajira na ulimwengu unaobadilika;
18. Angalau mtu mmoja katika kila watanzania wawili wenye sifa za kuajiriwa kuwa wameajiriwa katika sekta rasmi na wakiwa na mikataba kamili ya ajira;
19. Watanzania wote wanafurahia uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kukusanyika katika mazingira ya amani, usalama na utulivu; na
20. Ardhi yote ya Tanzania kupangwa na kupimwa kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo ardhi kwa ajili ya makazi bora, kilimo, mifugo na uwekezaji.

## MUUNDO WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

Dira 2050 imegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:

1. **Msingi Mkuu**: utawala, amani, usalama na utulivu. Eneo hili ndiyo jiwe la msingi la Dira 2050 linalobeba maeneo mengine. Kwa mantiki hiyo, kuyumba kwa eneo hili kutasababisha kuyumba kwa maeneo mengine yote ya Dira.
2. **Nguzo**: kuna nguzo tatu zinazobeba Dira 2050: uchumi imara, jumuishi na shindani; uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; na uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Kufikiwa kwa malengo ya Dira kunategemea ufanisi katika utekelezaji wa nguzo hizi.
3. **Vichocheo**: ni maeneo yanayochochea kasi ya utekelezaji wa maeneo mengine ya Dira ili kuleta tija, ufanisi na ubunifu.
4. **Sekta za Kimageuzi**: hizi ni sekta za kipaumbele ambazo utekelezaji wake unatarajiwa kuchagiza na kuwezesha ukuaji wa uchumi kufikia lengo la taifa la kuwa na uchumi wa kati ngazi ya juu.

Muhtasari wa muundo wa Dira 2050 umeoneshwa katika Kielelezo Na.1.




Kielelezo 1: Muundo wa Dira 2050

## Msingi Mkuu wa Dira: Utawala, Amani, Usalama na Utulivu

Lengo la Msingi Mkuu wa Dira ni kuwa na mifumo imara ya kisheria na kitaasisi katika kuwezesha utekelezaji endelevu na wenye ufanisi wa Dira 2050.

Maeneo yatakayozingatiwa:

1. **Utawala bora na haki ya jamii** katika ngazi mbalimbali za serikali na tasisi na mifumo yote ya kijamii itakayochagizwa na kuwepo kwa utawala wa sheria; demokrasia; kupinga unyanyasaji wa aina zote, kupiga vita dhidi ya rushwa; na kudumisha uhuru wa taasisi za kiraia.

2. **Serikali imara za mitaa na zenye ufanisi**, zinazojitegemea, zenye ubunifu, zinazozingatia maadili ya utumishi na zinazowajibika, na kutoa huduma bora kwa jamii.

3. **Uwajibikaji katika utumishi wa umma**: sifa hii inaongozwa na matamanio yafuatayo: kuwepo kwa utumishi wa umma wenye maadili, unaozingatia weledi na utawala wa sheria. Vile vile Dira inasisitiza umuhimu wa raia kuzingatia sheria na kupiga vita maovu.

4. **Amani, usalama, na utulivu** ambayo ina matamanio yafuatayo: kuwepo kwa taifa imara na tulivu; lenye umoja licha ya tofauti za dini, kabila, jinsia; uwezo wa kubaini fursa na kutabiri matukio mapema ili kuweka mifumo madhubuti ya kujikinga na majanga na kulinda maslahi ya taifa.

## Nguzo ya Kwanza: Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Lengo la nguzo hii ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuimarisha ushindani na uwazi na kuwezesha utabiri wa sera za kiuchumi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kufikia uchumi imara, jumuishi na endelevu.

Maeneo yatakayozingatiwa katika nguzo hii ni haya yafuatayo:

1. **Sera za fedha, mapato, na kodi zenye kutabirika** zitakazozingatia uwiano katika vigezo muhimu kama vile mapato na matumizi, urari, akiba na uwekezaji, uzalishaji na mahitaji.

2. **Ubunifu katika vyanzo mseto vya mapato.** Katika eneo hili matamanio ni kuimarisha ushiriano wa sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na soko la fedha na mitaji katika kugharamia shughuli za maendeleo.

3. **Mazingira yenye kuvutia, kulinda na kuendeleza uwekezaji na biashara** yatakayowezesha kuwepo kwa sera endelevu na zinazotabirika, na kupunguza gharama za uwekezaji na biashara.

4. **Mashirika ya umma ya kimkakati** kuwa na mashirika ya umma madhubuti na yenye ufanisi yenye kuzingatia uadilifu, uwazi, na uwajibikaji. Pia yanapaswa

kufanya kazi kwa uhuru, kuvutia uwekezaji mbalimbali, na kuzingatia faida ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na utoaji wa huduma za umma.

5. **Sekta binafsi imara** yenye nguvu na kushirikiana na Serikali ambayo itachagiza maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

6. **Ushirikiano wa kimkakati wa kikanda na kimataifa** wenye lengo la kuleta mafanikio ya kiuchumi, kukuza masoko, uwekezaji na teknolojia.

## Nguzo ya Pili: Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

Lengo la nguzo hii ni kuwezesha ujenzi wa rasilimali watu wenye maarifa, ujuzi stahiki, motisha na uwezo wa kushindana kimataifa, na kuendeleza jamii.
Maeneo yatakayozingatiwa katika nguzo hii ni haya yafuatayo:

1. **Jamii iliyoelimika, yenye ujuzi, na inayojiendeleza,** ili kuchangia katika kuleta maendeleo ya taifa, kukabiliana na changamoto, na kuhimili ushindani katika ngazi za kikanda na kimataifa.

2. **Jamii yenye afya** inayozingatia kanuni za afya ikiwa ni pamoja na kinga, huduma za afya zenye ubora na nafuu, lishe bora, vyakula na dawa zilizo salama.

3. **Hifadhi ya jamii jumuishi** inayohakikisha upatikanaji wa bima ya afya kwa wote, ulinzi dhidi ya uonevu na unyanyasaji hususan kwa watoto, wanawake na watu wenye ulemavu, mfumo wa hifadhi unaolenga kuondoa umaskini uliokithiri.

4. **Viwango bora vya maisha** kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora, maji safi na salama, nishati safi na nafuu, na mazingira salama.

5. **Nguvukazi yenye uwezo na motisha.** Matamanio katika eneo hili ni: kuwa na uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na idadi ya watu; kukuza vipaji kwa vijana; kulinda talanta na utaalamu kwa kuweka mazingira mazuri ya kuzibakiza nchini; kujenga jamii inayoheshimu uwazi na ushindani ili kujiendeleza; kuwa na sera na sheria rafiki za kazi.

6. **Jamii yenye mshikamano inayowajibika na shirikishi**. Kujenga jamii inayoshiriki katika maamuzi yanayowahusu na inayojishughulisha na masuala ya kijamii katika maeneo yao na taifa kwa ujumla; kukuza uzalendo na mshikamano wa kitaifa.

## Nguzo ya Tatu
## Uhifadhi wa Mazingira na Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Lengo ya nguzo hii ni kufikia maendeleo endelevu yanayozingatia uhifadhi wa mazingira, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa, na kujenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Maeneo yatakayozingatiwa katika nguzo hii ni haya yafuatayo:

1. **Uhifadhi wa bioanuai**: Ustawi wa wanyamapori na mimea katika mazingira ya asili kwa manufaa ya uchumi wa nchi na maendeleo ya jamii kwa kizazi cha sasa na kijacho.
2. **Uhifadhi wa ardhioevu na rasilimali maji**: Ardhioevu bora zitakazotoa huduma kwa manufaa ya kijamii, kiuchumi; na utunzanji wa vyanzo vya maji kama rasilimali muhimu na ya pekee kwa jamii.
3. **Udhibiti wa uchafuzi wa mazingira**: Kujenga jamii yenye mwamko na weledi katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira.
4. **Usimamizi endelevu wa ardhi:** Usimamizi madhubuti na endelevu wa rasilimali ardhi, ikijumuisha upimaji ardhi na upangaji wa makazi, kuwa na majiji na miji ya kijani, safi na endelevu, kwa ajili maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
5. **Uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi:** Kujenga taifa lenye uwezo wa kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari za majanga kwa maendeleo endelevu.

## VICHOCHEO VYA DIRA

Dira 2050 imeanisha vichocheo vitano (5) vifuatavyo:

1. **Usafirishaji Fungamani:** Usafirishaji fungamani unahusisha kuoanisha mifumo ya uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi, usambazaji, na utoaji wa huduma, kwa lengo la kuongeza ufanisi. Hivyo ni muhimu kuimarisha mifumo ya usafiri na kuwa fungamanishi ili kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi. Tanzania inadhamiria kuwa lango kuu la biashara katika kanda ya Mashariki, Kati and Kusini mwa Afrika ikinufaika na fursa iliyonayo ya kijiografia kwa kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya usafirishaji na teknolojia inayofungamanisha shoroba za kiuchumi nchini, kuimarisha usafirishaji wa mizigo wenye ubora wa juu na kiwango cha kimataifa na mifumo ya udhibiti, na ukusanyaji mapato yenye ufanisi, uwazi na wezeshi.
2. **Sayansi na Teknolojia:** Tanzania kuwa taifa lenye uwezo na nguvu ya kiteknolojia, linalowekeza kwenye ukuaji endelevu, kuongeza maendeleo ya watu, na kukuza utawala bora, na kufungua njia ya baadaye yenye mafanikio na usawa. Dira 2050 inalenga kuchochea matumizi ya teknolojia katika shughuli za uzalishaji, hifadhi na usambazaji wa bidhaa na huduma pamoja na kutumia teknolojia zinazochipukia.
3. **Utafiti na Maendeleo**: Dira 2050 inatoa msisitizo wa kuwekeza katika tafiti na kutumia matokeo ya utafiti katika kuandaa sera na kufanya maamuzi katika sekta na ngazi mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Katika muktadha huu, Dira 2050 inadhamiria Tanzania kuwa kitovu cha ubunifu wa kikanda, vyuo vikuu vya kiwango cha kimataifa na vituo bora vya utafiti kinachosaidia uvumbuzi wa ndani katika hatua zote, kuanzia wazo hadi biashara. Pia Dira inalenga kuwa na mfumo thabiti wa utafiti na maendeleo unaolinda hatimiliki na kuvutia ushirikiano wa kimataifa ili kuchochea uvumbuzi na uwekezaji.
4. **Mageuzi ya Kidijitali**: Mabadiliko ya kidijitali yanaweza kuisukuma Tanzania kufikia malengo yake ya mwaka 2050 kwa kuimarisha ukuaji wa uchumi, kuboresha utoaji wa huduma, na kukuza ubunifu kupitia teknolojia za kidijitali. Hivyo basi, Dira 2050 inakusudia yafuatayo; Tanzania kuwa kitovu cha kikanda kinachoongoza kwa uundaji wa maudhui ya kidigitali, kwa matumizi ya ndani na nje; kuwa kitovu cha kikanda cha maendeleo ya teknolojia ambacho kinatumia teknolojia zinazochipukia kama akili unde (artificial intelligence), blockchain, na mtandao wa vitu (Internet of Things) ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kuboresha utoaji wa huduma, na kuimarisha ushindani wa kimataifa. Pia Dira inadhamiria kujenga mfumo madhubuti, jumuishi wa utoaji wa takwimu za ubora na upatikanaji wa data za mara kwa mara, ambazo zimejumuishwa katika mifumo ya kitaifa na ya sekta ili kusaidia ufuatiliaji, tathmini, na maboresho ya programu za maendeleo.
5. **Nishati**: Mageuzi ya kiuchumi yanarajiwa kuchochewa na sekta za uzalishaji viwandani na huduma. Nishati ni kichocheo muhimu katika kusababisha mageuzi haya yatokee. Hivyo, serikali na wadau watawekeza katika kuhakikisha kuwa nchi ina nishati ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji, huduma na matumizi mengine.

## SEKTA ZA KIMAGEUZI

Dira 2050 imeainisha sekta za kipaumbele zenye nafasi ya kipekee katika kuchochea kasi ya mageuzi ya kiuchumi. Sekta hizi zitachaguliwa kwa kuzingatia sifa na vigezo vifuatavyo: **fursa ya kuzalisha ajira kwa kasi na wingi, kuongeza fedha nyingi za kigeni, na sekta fungamani zenye uwezo wa kuchagiza maendeleo ya sekta nyingine.**

Sekta za kimkakati zitaendelea kuchaguliwa kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa na mipango ya nchi kwa kipindi husika. Baadhi ya sekta za kimkakati zinazoweza kuchaguliwa ni:

1. **Kilimo**: Kilimo kuwa sekta ya kisasa, yenye tija, na ustahimilivu kwa kutumia teknolojia za kisasa, kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao, na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika. Tanzania kuwa ghala la chakula linaloaminika katika Afrika na kinara wa kimataifa katika mazao muhimu kama korosho, kahawa, mboga mboga, huku ikiboresha uzalishaji endelevu katika mifugo, uvuvi, na misitu.
2. **Huduma za Watumiaji:** Tanzania kuwa na sekta rasmi ya huduma za watumiaji yenye tija na ufanisi, inayoboresha maisha ya mtu mmoja mmoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa.
3. **Utalii:** Kuboresha na kupanua huduma za utalii nchini ~~wa~~ Tanzania, hususani utalii wa fukwe, mikutano, utalii wa meli, urithi na utamaduni. ~~na~~ Kuendeleza uhifadhi wa mazingira ili Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tatu bora barani Afrika kwa kuvutia na kutembelewa na idadi kubwa zaidi ya watalii; na kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika ukuaji wa uchumi.
4. **Madini:** Kuongeza thamani ya mazao ya madini ili Tanzania inufaike zaidi kiuchumi kwa kuimarisha sekta ya viwanda vya usindikaji. Kuwekeza katika kuongeza thamani ya madini muhimu kama lithiamu, grafaiti, na madini adimu (rare earth minerals), na kuhakikisha Tanzania inachukua nafasi ya kipekee katika mnyororo wa ugavi wa kimataifa wa teknolojia za kijani.
5. **Uzalishaji Viwandani:** Kuimarisha sekta ya viwanda kwa kupanua usindikaji wa mazao ya kilimo, uzalishaji wa vyakula, na bidhaa za viwandani. Kuwekeza katika nishati safi kwa uendeshaji wa viwanda, kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje, na kujenga msingi imara wa viwanda shindani, endelevu, na wenye utofauti wa uzalishaji.
6. **Huduma za Fedha:** Kuongeza kasi ya kutoa huduma za kifedha jumuishi kwa kuwafikia asilimia 90 ya wananchi kupitia maendeleo ya benki za kidijitali, upatikanaji rahisi wa mikopo, na kuhamasisha uwekezaji. Hatua hizi zinalenga kuimarisha biashara ndogo ndogo na za wastani na kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi katika maeneo yote ya Tanzania.

7. **Ujenzi na Mali Zisizohamishika**: Makaazi yenye hadhi na endelevu kwa kila Mtanzania na ukuaji wa miji kupitia uwekezaji katika sekta ya mali isiyohamishika na kuvutia uwekezaji wa kigeni, kuboresha miundombinu.
8. **Uchumi wa Buluu:** Kutumia ipasavyo rasilimali za uchumi wa buluu wa Tanzania kwa kupanua uvuvi endelevu, kuendeleza miundombinu ya gesi asilia, na kuboresha bandari. Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya baharini katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.
9. **Michezo na Sanaa za Ubunifu**: Kuendeleza sekta ya michezo na sanaa kama chachu ya uwezeshaji wa vijana na ukuaji wa uchumi. Kuwekeza katika miundombinu ya kisasa, kukuza vipaji, na majukwaa ya kidijitali ili kufungua fursa za ajira na masoko ya ndani na kimataifa.
10. ***Sekta mtambuka*** ambazo ni kielelezo na msingi wa maendeleo ya watu: elimu, afya, hifadhi ya jamii, umiliki wa ardhi, maendeleo ya makazi, maji na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

## UTEKELEZAJI WA DIRA

Ili kutekeleza kwa ufanisi Dira ya Tanzania 2050, uwekaji wa vipaumbele vya kimkakati, mbinu zinazoendeshwa na ushahidi, na mifumo thabiti ya uwajibikaji na nidhamu ya utekelezaji ni muhimu kuzingatiwa. Kama mwongozo mkuu wa kitaifa unaoongoza kwa miaka 25 ijayo, ambapo sera zote za sekta, mipango na programu mbalimbali zioananishwe na malengo yake ili kuzuia kuwapo kwa utitiri wa dira za kisekta.

1. **Uwekaji wa Vipaumbele vya kimkakati:** Kutokana na rasilimali ndogo na malengo mapana ya Dira 2050, ni muhimu kuwa na vipaumbele bayana. Dira imebainisha vigezo muhimu vya kuzingatia wakati kuchagua sekta za kimageuzi zitakazochochea mageuzi ya kiuchumi na kijamii.

2. **Utekelezaji na Uratibu wa Awamu:** Dira 2050 itatekelezwa kupitia mipango ya maendeleo ya miaka mitano-mitano inayotokana na mpango elekezi wa miaka 25. Mipango hii ya miaka mitano-mitano itaongozwa na vipaumbele mahususi vitakavyozingatiwa katika utekelezaji wa kila mpango husika. Kwa upande mwingine, mipango hiyo itagawanyika katika vipindi vya utekelezaji vya mwaka mmoja mmoja.

   **2.1 Mikakati ya Kisayansi ya Utekelezaji:** Ili Dira ya 2050 itekelezwe kwa ufanisi, ni lazima kuwa na mikakati iliyoandaliwa kisayansi kwa kutumia data, uchambuzi wa mwenendo wa idadi ya watu; mahitaji ya rasilimali, na kuzingatia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

   ***2.2* Ufuatiliaji na Tathmini:** Ufuatiliaji, tathmini na uzoefu ni muhimu katika kutekeleza Dira 2050, kwani inapima hatua zinazofikiwa, uwajibikaji na uwezo wa kufanya mabadiliko.

   Ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini, ni muhimu kuwa na vigezo vya kupima ufanisi kwa kila sekta. Vigezo hivi vinawezesha ufuatiliaji sahihi wa hatua zilizofikiwa, kuonesha mafanikio na kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa malengo ya Dira 2050.

   Pamoja na ufuatiliaji na tathmini, ni muhimu kuwa na mfumo utakaotoa motisha kwa watendaji na taasisi zinazofanya vizuri, na kuchukua hatua kwa wale ambao hawatimizi wajibu wao ipasavyo. Mfumo huo utakuza utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii na kuimarisha uwajibikaji.

3. **Uratibu na Usimamizi wa Utekelezaji wa Dira:** Utekelezaji madhubuti wa Dira 2050 unahitaji uratibu thabiti na uwiano muafaka wa nafasi ya Serikali na ya sekta binafsi. Tume ya Taifa ya Mipango itakuwa mratibu mkuu wa kuainisha mikakati na rasilimali za kisekta na malengo ya Dira 2050, wakati huo huo ikihakikisha kuna ushirikiano thabiti na wadau wote husika. Njia hii itahamasisha utafutaji wa rasilimali wa pamoja, mawasiliano ya kimkakati na ushiriki mpana wa wadau, kuhakikisha kuwa juhudi zote zinawiana katika kutekeleza malengo ya Dira.